MTANDAO WA KUZUIA UKATILI WA KIJINSIAG

**Siku 16 za Unaharakati Dhidi ya Ukatili wa Kijinsia 2017**

**Mwongozo wa majadiliano kwa Njia ya Bango**

# KILA MSICHANA ANA THAMANI!

JE! UTACHUKUA HATUA GANI ILI KUWAWEZESHA WASICHANA KUBAKI SHULENI?

## KILA MSICHANA ANA THAMANI! JE! UTACHUKUA HATUA GANI ILI KUWAWEZESHA WASICHANA KUBAKI SHULENI?

Ndani ya kiti ya kampeni, bango la ukubwa wa A3 limejumuishwa. Unaweza kutumia bango hili kwa njia tofauti. Unaweza kulibandika katika sehemu za wazi kwenye jamii, ili wanajamii waone. Tunatarajia swali katika bango litachochea tathmini binafsi ndani ya wanajamii. Unaweza pia kupanua matumizi ya bango kwa kufanya majadiliano ya papo kwa hapo na majadiliano katika vikundi.

Majadiliano yanaweza kuwa yasiyoandaliwa au yaliyoandaliwa kabla. Kabla ya kuonyesha bango, unaweza kushirikisha watu walio karibu na eneo la majadiliano. Unaweza kurejea maswali yaliyo hapo chini ili kuwezesha majadiliano jinsi wasichana wanavyoweza kuungwa mkono ili kukamilisha elimu yao. Kuwa huru kutumia maswali yanayoweza kuwafaa washiriki katika mazingira yao.

Zifuatayo ni hatua muhimu za kuzingatia wakati unapotayarisha au kuwezesha majadiliano:

- Soma maelezo ya kampeni ili uweze kuifahamu kauli mbiu ya kampeni. Oanisha namna swala hili lilivyo katika jamii yako. Unaweza pia kupanua mjadala kwa kushirikisha swala hilo wafanyakazi wenzako.
- Fanya mazoezi au igiza unafanya majadiliano na watu wa timu yako kabla ya kwenda kwa jamii, hii itakusaidia kuandaa na kuwezesha majadiliano vizuri.
- Unaweza kufanya majadiliano na washiriki hadi 15 ili majadiliano yawe yenye tija. Majadiliano yanaweza kufanywa mahali popote katika jamii ambapo watu wanaweza kukusanyika na kuzungumza, kwa mfano chini ya mti, nje ya nyumba ya mtu, saluni, bar, nk.
- Waeleze washiriki kuwa hakuna jibu sahihi au lisilosahihi . Washukuru washiriki kwa michango yote waliotoa.
- Hamasisha majibu kutoka kwa washiriki wote, wape nafasi sawa ya kushiriki.
- Kumbuka usiwaambie washiriki nini cha kufikiria. Kuuliza maswali inaweza kuwa njia yenye nguvu zaidi kuliko kutoa ujumbe.
- Baada ya kukamilisha majadiliano, weka bango mahali litakapoonekana na kundi hilo.

## MASWALI YA MAJADILIANO YALIYOPENDEKEZWA

1. Unaona nini katika bango hili? Unapata ujumbe gani?
2. Fikiria juu ya wasichana katika jamii yako, je wote wanaenda shule? Ni wasichana wangapi wanaoweza kukamilisha masomo yao?
3. Je, ni mambo gani yanayowaathiri wasichana 'kutokamilisha elimu ya juu? (wahamasishe washiriki wafikiri kuhusu mila na desturi katika jamii pamoja na kanuni na sheria zilizopo shuleni)
4. Nini hutokea mwanafunzi wa kike akaolewa au kupata ujauzito? Je! anawezakuendelea na masomo yake? Je, anaweza kuendelea na masomo baada ya kujifungua? Ikiwa hapana, kwa nini?
5. Unajisikiaje pale wasichana wanapozuiwa kukamilisha elimu yao? Tafadhali toa sababu zinazokufanya ujisikie hivyo?
6. Kuna faida gani wasichana wengi wanapo fanikiwa kukamilisha elimu yao? (kwa mtu binafsi, ngazi ya kaya na jamii)
7. Ni hatua gani utakazochukua kama mtu binafsi / kikundi katika kusaidia wasichana wengi kubaki shuleni na kukamilisha elimu zao?
8. washukuru washiriki kwa muda na ushiriki wao na fanya hitimisho la wazo muhimu lililojitokeza:
    a. Wasichana wanakabiliwa na ubaguzi wanapojaribu kufikia na kukamilisha masomo yao, na ina athari mbaya kwa wasichana, familia zao na jamii.
    b. Vitendo vidogo utakavyofanya ili kumweka msichana shuleni vitaleta matokeo makubwa katika jamii yako kama vile: kupunguza Ukatili Dhidi ya Wanawake, kiwango cha vifo vya wanawake wajawazito na watoto wachanga.